

Mwafrika 19/7/63

MRENO APIGWA VIKALI GUINEA

Lisbon, Ureno, Alhamisi.

RIPOTI KUTOKA LISBON, MJI MKUU WA URENO
INADAI KUWA JESHI KUBWA LA WANANCHI
WANAOPIGANIA UHURU, LIMEVAMIA NA KUTE-
KA SEHEMU 15 KWA 100 YA PORTUGUESE GUINEA,
KOLONI LA KIRENO LILILO KATIKA AFRIKA YA
MAGHARIBI.

Jeshi hilo la wananchi
linasemekana limetoka ka-
tifa nchi huru za jirani za
Jamhuri ya Guinea na
Senegal.

Serikali ya Kireno ime-

kwisha kukubali kuwa jeshi
hilo la wananchi lime-
shika sehemu kubwa ya
Koloni lao la Portuguese
Guinea. Pia Ureno imeku-
bali kuwa Jeshi hilo la wa-
nanchi lina askari wengi
sana wenye silaha za kuto-
sha.

Mafanikio hayo ya jeshi la
wananchi wanaopigania uhuru,
yameogofisha sana Ureno yen-
yewe pamoja na majirani
wake, kama vile Spain. Wana-
yaona mashambulio hayo ndi-
yo mwanzo wa mashambulio
makubwa zaidi katika Mako-
loni mengine ya Kireno ya
Msumbiji na Angola.

Askari 27

Waziri wa Ulinzi katika Ure-
no, Manuel Gomes Daraujo,
amedai kuwa majeshi hayo
yanayopigania uhuru yame-
vamia, na kunyang'anya pa-
moja na kuuu watu katika
Portuguese Guinea.

Ameongeza kudai kuwa ka-
tika majeshi yake ni askari
27 tu waliokufa mpaka hivi
leo.

Lakini Mtaalamu wa Kihis-
pania, nchi iliyo jirani na
ndugu wa Ureno, amesema
kuwa majeshi ya Kireno kati-
ka Koloni lake la Guinea ni
ndogo sana na haliwezi kuzuia
mashambulio makali kama
hayo.

Mtaalamu mwingine wa Ki-
hispania katika mambo ya
Afrika, amesema kuwa mash-
ambulio katika Angola yataku-
wa kitu kingine na huweza
kuleta mgongano mkubwa ka-
tika Afrika.